

1. Mgeni

Akiwa amechoka na huku amebeba kiriba cha maji mgongoni, mwanada- da huyo alikuwa akielekea nyumbani kwake akiwa mlegevu, na wanawe wachanga wakiwa wanamsubiri mama mzazi awasili.

Alipokuwa njiani mwanadada huyo alikutana na mgeni aliyemsaidia kube- ba kile kiriba cha maji. Punde si punde waliwasili nyumbani kwa dada huyo. Baada ya mlango kufunguliwa watoto walimuona mama na mgeni ambaye aliteremsha kiriba cha maji na akasema:

“Naam, yaonekana kwamba hamna mtu yeyote wakuwatekea maji! Imekuwaje hadi mkawa na upweke kiasi hiki?”

Mwanadada huyo alijibu kwa huzuni: “Mume wangu alikuwa mwanajeshi; Ali (a.s) alimtuma kwenye mstari wa kwanza vitani, na ndipo alipouwawa. Na hivi sasa nimebaki mpweke na watoto hawa.”

Mgeni huyo alikata kauli na hakuendelea kuzungumza zaidi. Aliinamisha kichwa chake na akaondoka. Lakini wazo la mjane na mayatima waliokuwa hawajiwezi halikumtoka.

Na ikawa ndio sababu ya kutolala usiku huo. Kulipokucha, mgeni huyo alichukua kapu lake, na ndani yake akaweka kipande cha nyama, unga, na tende. Kisha moja kwa moja alielekea hadi nyumbani kwa mjane yule na kubisha mlango.

“Ni nani wewe?”

“Ni mimi yule bwana aliyekubebea maji jana. Na hivi sasa nimewaletea watoto vyakula.”

“Mwenyezi Mungu (swt) akujaalie kila la kheri na ahukumu baina yetu sisi na Ali.”

Kisha mwanadada huyo alifungua mlango na kumpokea bwana huyo. Alipoingia, alitamka na kusema:

“Natamani kutenda mema. Ima uniruhusu nikande unga na nipike mikate, au uniruhusu niwaangalie watoto.”

“Nashukuru, lakini nadhani nina ujuzi wa kupika zaidi yako. Wewe waangalie watoto hadi nitakapomaliza

upishi.”

Bila kupoteza muda mwanadada huyo alielekea kukanda unga na bwana huyo alianza kumega nyama aliyoleta na kuwalisha watoto. Wakati alipokuwa akiweka tonge la chakula mdomoni mwa kila mmoja wao alikuwa akisema:

“Mwanangu msamehe Ali kama hakuweza kutekeleza wajibu wake juu yako!”

Unga ulipokuwa tayari kupikwa; mwanadada yule aliita: “Ewe bwana mungwana washa jiko tafadhali.” Bwana huyo alifanya hivyo. Moto ulipowaka alisogeza uso wake karibu ya moto na kusema, “Onja joto la moto.” Hii ndiyo adhabu ya wale walioshindwa kutekeleza wajibu wao kwa mayatima na wajane.”

Kwa bahati, mwanamke mmoja aliyekuwa jirani aliingia na baada ya kum- tambua mgeni huyo alitirikwa na machozi. “Ah! Kwani haumtambui huyu bwana anayekusaidia? Yeye ndiye Amirul-Muuminiin (Kiongozi wa waumini) Ali bin Abi-Talib (a.s).”

Mjane huyo alisogea mbele huku akilia kwa kuona haya “Laana na aibu iwe juu yangu. Naomba msamaha wako.”

Hapana, mimi ndiye naomba msamaha kwa kutotimiza wajibu wangu juu yenu.”

Source URL: <https://www.al-islam.org/node/24937>